**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**JESHI LA POLISI TANZANIA**

Anwani ya Simu: "MKUU POLISI"
Simu Namba: 026 2323585
Fax: 026 2323586
E – Mail: info.phq@tpf.go.tz

Ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi,
Makao Makuu ya Polisi,
4 Mtaa wa Posta,
S. L. P. 961,
**40483 DODOMA**

28/06/2024

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU WATU BINAFSI, KAMPUNI AU TAASISI ZINAZOMILIKI SILAHA KINYUME CHA SHERIA

Jeshi la Polisi linapenda kuutarifu umma juu ya masuala matano yanayohusiana na umiliki wa silaha. Masuala hayo ni;

1. **Kampuni binafsi za ulinzi kutumia silaha zilizotengenezwa kienyeji (Gobore) kinyume cha Sheria**.

Mtakumbuka kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria Namba 2 ya Udhibiti wa Silaha na Risasi ya Mwaka 2015 sambamba na kufuta Sheria ya Silaha na Risasi ya Mwaka 1991 kwa lengo la kukidhi mahitaji ya sasa ya kukabiliana na changamoto za kumiliki na kusambaa kwa silaha haramu. Kutungwa kwa Sheria hii kulikwenda sambamba na marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa sura ya 290 kwa kuondoa kifungu 7(1) (L) kilichokuwa kinazipa Halmashauri na Manispaa Mamlaka ya kukusanya mapato yatokanayo na leseni za silaha aina ya Gobore ambapo kufuatia kutungwa kwa Sheria mpya, jukumu hili lilipewa Jeshi la Polisi.

Hata hivyo katika siku za karibuni, Jeshi la Polisi limebaini kuwepo kwa baadhi ya kampuni binafsi za ulinzi ambazo zinamiliki silaha aina ya Gobore bila kuwa na vibali kinyume na utaratibu wa sheria unaozitaka kampuni za ulinzi kumiliki shotgun kwa ajili ya shughuli za ulinzi. Aidha, ikumbukwe kuwa wananchi waliokuwa wakimiliki silaha aina ya Gobore kwa kutumia leseni zilizotolewa na Halmashauri za Miji na Manispaa, walielekezwa kuendelea kulipia silaha zao katika Ofisi za Wakuu wa Polisi Wilaya (OCD) mpaka watakapoamua kutoendelea kumiliki au kutokana na sababu nyingine ikiwemo kufariki na kwamba silaha hizo hazitamilikishwa kwa watu wengine tena bali Jeshi la Polisi litaziondosha kwa kuziteketeza.

Kutokana na hilo, wamiliki wa kampuni binafsi za ulinzi wanafahamishwa kuwa ni marufuku kutumia silaha aina ya Gobore kwa kazi za Ulinzi na wanaofanya hivyo wanaelekezwa kuacha mara moja kwani ni Kinyume cha Sheria. Wamiliki hao wanashauriwa kufuata utaratibu wa kisheria wa kumiliki silaha aina ya Shotgun kwani ndizo zinazoruhusiwa kutumika kwa shughuli za ulinzi.

Jeshi la Polisi linatoa muda wa miezi miwili kuanzia tarehe 1/7/2024 hadi 31/8/2024 na baada ya kipindi hicho kutakuwa na msako mkali ambapo Kampuni binafsi ya ulinzi itakayokutwa ikimiliki silaha hizo itachukuliwa hatua za kisheria.

2. **Silaha za mirathi**.

Kwa mujibu wa kifungu cha 55 cha Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi ya Mwaka 2015 ni kwamba mmiliki wa silaha mara anapofariki, ndugu wa marehemu wanapaswa kuisalimisha silaha hiyo katika kituo cha Polisi kilicho karibu wakati taratibu za mirathi na umilikishwaji kwa mtu mwingine kwa mujibu wa Sheria zikiendelea.

Hivyo Jeshi la Polisi linawakumbusha wananchi kusalimisha silaha zilizokuwa zinamilikiwa kihalali na ndugu zao ambao kwa sasa ni marehemu, ili silaha hizo zisilete madhara katika jamii. Watambue kuwa kuendelea kuhifadhi silaha hizo nyumbani ni kinyume cha Sheria na yeyote atakayepatikana akimiliki silaha hizo atakuwa ametenda kosa na endapo akipatikana na hatia mahakamani, anaweza akapewa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka kumi na tano jela au faini ya shilingi milioni kumi au vyote kwa pamoja.

3. **Wamiliki wa silaha wasiolipia ada za leseni zao za kumiliki silaha.**

Kwa mujibu wa Kanuni namba 16 na 20 ya Kanuni za Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi za Mwaka 2016, mmiliki wa silaha anapaswa kulipia ada ya leseni yake kila ifikapo mwezi Julai kila Mwaka. Hata hivyo wapo baadhi ya wamiliki wa silaha ambao wamekuwa hawalipii leseni zao kwa miaka kadhaa bila kuwa na sababu za msingi.

Kutokana na hilo, Jeshi la Polisi linatoa miezi mitatu kuanzia tarehe 01 Julai 2024 hadi tarehe 30 Septemba 2024 ili kuwapa nafasi wananchi wanaomiliki silaha kulipia ada na madeni ya leseni zao. Baada ya muda huo kupita wamiliki ambao watakuwa hawajalipa ada ya mwaka 2023/2024 pamoja na madeni ya ada za miaka ya nyuma watafutiwa leseni zao kwa mujibu wa Kifungu cha 8 (1) (b) cha Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi ya Mwaka 2015.

Aidha, katika maonesho ya 48 ya Sabasaba ya Mwaka 2024, Jeshi la Polisi litakuwa na Dawati la Umiliki wa silaha ambapo wamiliki wa silaha watapewa namba za malipo kwa ajili ya kulipia ada pamoja na madeni ya leseni kulingana na kiasi wanachodaiwa.

**4. Umiliki wa silaha bandia (Toy guns)**

Jeshi la Polisi linapenda kuwafahamisha watanzania kuwa, silaha bandia haziruhusiwi kumilikiwa na mtu, taasisi au kampuni yoyote. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 70 cha Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi ya Mwaka 2015. Zuio la umiliki wa silaha hizi umetokana na ukweli kwamba ni kinyume cha sheria na kwamba silaha hizo zimeshawahi kutumika katika kutenda uhalifu hasa unyang'anyi wa kutumia silaha. Hivyo wananchi wote wanaomiliki silaha bandia wazisalimishe silaha hizo katika vituo vya Polisi kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa dhidi yao.

**5. Silaha zisizo na maafa (Non-Lethal Weapons).**

Hivi karibuni kumeibuka baadhi ya wananchi kutaka kuingiza nchini silaha zisizo na maafa kwa ajili ya kuendesha michezo ya ulengaji shabaha. Silaha hizi zimeainishwa chini ya kifungu cha 69 (1)(a-h) cha Sheria ya Udhibiti wa silaha na risasi ya mwaka 2015.

Vile vile, kanuni namba 38 ya Sheria hiyo imeweka zuio la uingizaji wa silaha hizo isipokuwa kwa Amri ya Waziri mwenye dhamana baada ya kushauriana na Bodi ya Taifa ya Ushauri na Udhibiti wa Silaha za Kivita. Hivyo, wananchi watambue kuwa silaha zisizo na maafa haziruhusiwi hapa nchini isipokuwa kwa kibali maalum.

Kwa mantiki hiyo Jeshi la Polisi, halitasita kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote au kikundi cha watu watakaopatikana wakimiliki silaha hizo kinyume cha Sheria ikiwa ni pamoja na kukiuka maelekezo yaliyotolewa kwenye namba moja hadi tano hapo juu.

**Imetolewa na**:
David A. Misime – DCP
**Msemaji wa Jeshi la Polisi**
Makao Makuu ya Polisi
Dodoma,Tanzania